JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS: TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO

SHULE YA SEKONDARI MLONGWEMA,
S.L.P 173,
LUSHOTO.

Kumb.Na**:MSS/JI/ADV/V.1/2021/1**

----------,

----------,

FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2021/2022 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MLONGWEMA

SEHEMU A: UTANGULIZI

1. Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka 2021/2022katika shule ya Sekondari Mlongwema, Tahasusi ya ……..
2. Shule ya sekondari Mlongwema ipo Mlola umbali wa kilometa 46, kaskazini mwa mji wa Lushoto. Ufikapo Lushoto mjini utapanda magari yanayoelekea Mlola kwa nauli ya shilingi elfu tano (5,000/=) tu. Ukifika Mlola panda pikipiki kwa shilingi elfu moja (1,000/=) tu hadi shuleni.
3. Shule ya sekondari Mlongwema ni shule ya bweni kwa wasichana tu kwa kidato cha tano na sita.
4. Ukiwa Mlongwema Sekondari, utalazimika kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu za Shule (kamilisha kiambatanisho B na C).
5. Utaripoti shuleni tarehe **05/07/2021** bila kuchelewa. Hata hivyo, Kama Serikali itatangaza tarehe nyingine tofauti na hii, utatakiwa kuripoti kwa kwa kuzingatia tarehe ya Serikali.
6. Fika na nakala ya cheti cha kuzaliwa na nakala ya ***Result slip siku ya Kuripoti.*** Kama huna cheti cha kuzaliwa, nenda Mahakamani ili **Uape upewe** ***Affidavit***, kuwa wewe ni raia wa Tanzania.

SEHEMU B: SARE YA SHULE NA MAHITAJI MENGINE

NB: KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA MKUU WA SHULE

NA.	SARE/MAHITAJI	MAELEZO
1	Mashati 2 meupe ya Mikono Mifupi,Tetroni (Lisiwe linalo bana au linalo onesha ndani)	Anunue duka lolote
2	Sketi 2 zinazovuka magoti za heshima za rangi ya Bluu iliyokolea (Dark Blue) mshono uwe wa V mbele.	Zinapatikana duka la shule
3	Masweta 2 ya rangi ya kijani iliyokolea (dark green) ya V (yasiwe ya vifungo)	Yanapatikana duka la shule
4	Sweta au jacket zito jeusi 01 lisilo na kofia, picha wala maandishi yoyote	Anunue duka lolote
5	Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2 vya kufunga na kamba (visiwe vyenye visigino virefu), na soksi nyeupe jozi 2.	Anunue duka lolote
6	Skafu moja ya rangi ya bluu iliyo kolea (dark blue)	Inapatikana duka la shule
7	Shuka 2 za rangi ya pink, Blanketi moja au mashuka mazito ya kujifunika, foronya mbili na chandarua moja ya rangi nyeupe.	Anunue duka lolote
8	Magauni mawili ya rangi ya kijivu (Grey) yawe ya kitambaa kizito kisichoonyesha nguo za ndani.	Yanapatikana duka la shule
9	Godoro imara la ukubwa wa futi mbili na nusu kwa sita ($2^1/_2$ x 6). (Godoro Dodoma au Comfy)	Linapatikana shuleni kwa Tsh. 10,000/= kwa muhula fedha hii inalipwa shuleni
10	Picha 4 za passport size	Apige popote
11	Picha nne passport size za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu	Apige popote
12	T – shirt 2 za rangi ya bluu ya mawingu isiyo na maandishi yoyote	Vinapatikana duka la shule
13	Tracksuit ya rangi ya bluu ya mawingu (light or sky blue) na raba nyeupe kwa ajili ya michezo.	Vinapatikana duka la shule
14	Sanduku imara la bati (tranker) kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyako	Anunue duka lolote
15	Vifaa vya chakula ikiwa ni pamoja na Kijiko,sahani, kikombe na bakuli	Anunue duka lolote ila visiwe vya plastiki
16	Ndoo ndogo moja na kubwa moja	Zinapatikana duka la shule
17	Vifaa vya usafi vikiwa ni pamoja na jembe 1 lenye mpini, mopper 1(ndoo na mopper), hard broom 1, fagio la chelewa 1 na fyekeo 1.	Anunue duka lolote

NB: Vifaa vinavyopatikana shuleni ni kwa sababu ya kurahisi wa huduma na kuepusha gharama zisizo za lazima wakati wa kusafiri.

SEHEMU C: VIFAA VYA DARASANI

1) Ufike na daftari za kutosha kwa masomo 4 utakayo soma,kalamu na mkebe (Mathematical Set) na scientific calculator kwa watakaosoma somo la jiografia.
2) Dictionary 1 ya kingereza kwa kingereza, kamusi ya kiswahili 1 na ya kiswahili kwa kingereza 1 kwa matumizi binafsi na kwa masomo ya tafsiri na ukalimani kwa somo la kingereza na kiswahili.
3) Karatasi kwa ajili ya mitihani (Rimu 2-A4)

SEHEMU D: ADA NA MICHANGO MINGINE

(LIPA KWENYE AKAUNTI YA NMB NAMBA 41603500042 YENYE JINA LA MLONGWEMA SECONDARY SCHOOL FUND)

1	Ada kwa mwaka	70,000
2	Kitambulisho cha mwanafunzi	6,000
3	Tahadhari (hairudishwi)	5,000
4	Nembo ya shule	2,000
5	Kuboresha Taaluma	20,000
6	Mtihani wa kujipima(Mock)	20,000
7	Afya na huduma ya kwanza kwa mwaka	10,000
8	Mishahara ya vibarua wa Shule (walinzi, wapishi nk), kwa mwaka	30,000
9	Uboreshaji mazingira ya kufundishia na kujifunzia, kwa mwaka	25,000
	JUMLA	**188,000**

MUHIMU:

1. Mwanafunzi aje na risiti ya malipo bank pay in slip (**BPS**)
2. Mwanafunzi atapokelewa tu iwapo amekamilisha kulipa ada, michango mingine na kukabidhi vifaa vyote vilivyoagizwa.
3. Mwanafunzi anashauriwa kuwa awe na fedha za mfukoni (pocket money) kwaajili ya kujikimu.
4. Ukifika shuleni ripoti moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule kisha taratibu nyingine zitafuata.
5. Hakikisha unasoma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Kuhusu vitabu vya kununua mwanafunzi ataelekezwa atakapofika shuleni.
Karibu sana Shule ya Sekondari Mlongwema.

CATHERINE W. MAPUNDA
MKUU WA SHULE
SIMU: 0767 555094/0620 555099

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI
MLONGWEMA LUSHOTO

KIAMBATANISHO A

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI MLONGWEMA

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1. HESHIMA

a) Mwanafunzi atasimama kumsalimia mwalimu na mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
b) Mwanafunzi atatumia lugha safi (inayokubalika) wakati wowote kati yake na wenzake, walimu au kwa mtu mwingine akiwa shuleni au nje ya shule.
c) Mwanafunzi atatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote wa shule kama walezi wake.
d) Mwanafunzi ataitika wito mara moja na kukimbilia aliko Mkuu anayemwita
e) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu kazi yoyote anayopewa na Mwalimu au Mlezi na anatakiwa ashirikiane na wenzake ili kufanya kazi hiyo.
f) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu **Bendera** ya Taifa, **Wimbo** wa Taifa, **Picha** za viongozi wa Serikali, **Nembo** ya Taifa na **Fedha** za Taifa.
g) Mwanafunzi atasimama katika mstari wakati wowote anaposubiri kupata huduma.
h) Mwanafunzi atakaa kimya (bila kelele) wakati wowote akiwa darasani au sehemu muhimu ya wito na asitoke nje ya darasa au eneo la shule bila ruhusa ya Mwalimu. Atatoka nje ya eneo la shule kwa siku zilizotangazwa au ruhusa tu.

2. MAHUDHURIO

a) Mwanafunzi anatakiwa ahudhurie vipindi vyote vya darasani kwa muda wote wa masomo. Na anatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zote zilizopangwa na anapokosa siku hata moja akifika akatoe taarifa kwa mmoja wapo wa hawa:
   i. Mwalimu wa zamu siku hiyo.
   ii. Mwalimu wa darasa.

iii. Makamu Mkuu wa Shule

b) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama vile Baraza la Shule, Ukaguzi wa usafi na Kupandisha Bendera ya Taifa.
c) Mwanafuzi atatakiwa kuwahi shughuli zote shuleni kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya shule. Tena anatakiwa kuwahi anapotakiwa au anaposikia kengele.
d) Mwanafunzi anatakiwa kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote anayopewa na Mwalimu wa somo darasani. Akikosa zoezi, jaribio au mtihani wowote akamuone mwalimu wa somo na Mwalimu Mwandamizi Taaluma.

3. SARE ZA SHULE NA USAFI

a) Mwanafunzi atatakiwa kuwa katika sare za shule zinazoruhusiwa kwa eneo husika na muda husika, muda wote ndani ya shule na nje ya shule na zikiwa katika hali ya usafi.
b) Mwanafunzi **hatoruhusiwa** kuvaa nguo yoyote amabayo haijaainishwa kama sare ya shule ndani na nje ya shule.

MAKATAZO:

4. SEHEMU ASIZORUHUSIWA KUTEMBELEA MWANAFUNZI

a) Mwanafunzi asitembelee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali/ruhusa maalumu
   i. Ofisi ya Walimu
   ii. Maabara
   iii. Nyumba za walimu au wafanyakazi wengine wa shule
b) Mwanafunzi **HARUHUSIWI KABISA** kutembelea sehemu hizi;
   i. Vilabu vya pombe
   ii. Nyumba za starehe
   iii. Nyumba za kufikia wageni
c) Mwanafunzi hatoruhusiwa kutoka nje ya shule isipokuwa kwa kibali au ruhusa maalumu

5. NI MARUFUKU:

a) Kuiba mali ya mtu binafsi au umma.
b) Kufanya uasherati, ubakaji au ushoga
c) Kulewa kilevi cha aina yoyote au kuvuta sigara au bangi.
d) Kupiga au kupigana.
e) Kuharibu mali ya umma au kujaribu kuharibu.
f) Kuoa au kuolewa

g) Mwanafunzi kumiliki simu shuleni au kuwa na kiashiria chochote cha kumiliki simu kama vile laini, vocha, chaja, betri ya simu na vingine vyote vinavyohusiana na simu.

ANGALIZO

Ni jukumu la mwanafunzi kufuata sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa pamoja na nyingine atakazoelekezwa ili kuepuka adhabu na kufukuzwa shule.

Walimu shuleni ni waelekezaji, walezi, waelimishaji na washauri wa wanafunzi.

Mwanafunzi akiwasikiliza atafika kule anakotarajia/anakopanga kufika Mtu hawezi kudai kuwa anaelimika wakati hana tabia inayokubalika katika jamii yake. Licha ya elimu yake mtu huyu atakuwa '**msungo'**

KIAMBATANISHO B

The united Republic of Tanzania

President's Office: Regional Administration and Local Government

Mlongwema Secondary School,
P.O BOX 173,
Lushoto.

_____

To the Medical Officer,
……,
……,
……...
……

Ref: A PUPIL'S MEDICAL EXAMINATIONS FORM

Please, examine the Pupil …… in respect of these areas and any other area(s) deemed fit Please. Delete whichever applies.
Does the Pupil have problems in connection with ……?

a) Sight Yes/No. If yes, state……
……
……

b) Hearing. Yes/No. If yes, state ……
……
……

c) T.B or any other Chronic Diseases. Yes/No. If yes, state …
……
……

d) Blood Pressure. Yes/No. If yes, state
……
……

e) Any Physical Impairment(s). Yes/No. If yes, state …
……
……

f) Do you therefore recommend this pupil to pursue studies at this school?
……

Name……..Signature…… Date: ……

Official Title…….. Official Stamp……

KIAMBATANISHO C

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO
SHULE YA SEKONDARI MLONGWEMA

I: TAARIFA ZA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI: ……
2. TAREHE YA KUZALIWA: ……..
3. URAIA: ……
4. DINI: ……
5. SHULE ULIYOSOMA: -
   JINA LA SHULE: ……..
   MWAKA WA KUANZA: …….. MWAKA WA KUMALIZA: ……..

SAHIHI YA MWANAFUNZI: …….. TAREHE: ……..

II: MAELEZO YA MZAZI /MLEZI WA MWANAFUNZI KUKIRI NA KUKUBALIANA NA SHERIA KANUNI NA KULIPA ADA, MICHANGO MINGINE NA MAELEKEZO MENGINE YA SHULE

1. JINA LA BABA MZAZI/MLEZI: ……..……
   MKOA: ……..…….. WILAYA: ……..……KATA: ……..……
   KIJIJI/MTAA:……..S.L.P……..……...SIMU……..……
   KAZI YA MZAZI/MLEZI: ……
2. JINA LA MAMA MZAZI/MLEZI: ……..…
   MKOA: ……..…….. WILAYA: ……..……KATA: ……..……
   KIJIJI/MTAA:……..S.L.P……..……...SIMU……..……
   KAZI YA MZAZI/MLEZI: ……

MAELEZO YA MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI

Mimi…….. ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……nimesoma na kuelewa maelezo yote yaliyotolewa kuhusu sheria, kanuni, ada na michango ya shule. Ninakubali mwanangu ajiunge na shule ya Sekondari Mlongwema na ninaahidi kulipa ada na michango hiyo pamoja na kutekeleza maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ikiwa ni pamoja na kutompatia mwanafunzi simu na endapo atabainika kuwa na simu anastahili kufukuzwa shule kwa mujibu wa kanuni na sharia za shule.

Jina…….. Saini……
Tarehe……